TANGAZO LA SERIKALI NA. 76 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE MAGARI MATATU YANAYOINGIZWA NCHINI NA WIZARA YA KILIMO KWA AJILI YA KUIMARISHA UWEZO WA WADAU WA MAENDELEO WA SEKTA LA MCHELE YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye Magari Matatu Yanayoingizwa Nchini na Wizara ya Kilimo kwa Ajili ya Kuimarisha Uwezo wa Wadau wa Maendeleo wa Sekta ya Mchele ya mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika kuanzia tarehe 16 Novemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa magari yaliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii, yanayoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha yatakayotumika na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya mradi wa kuimarisha uwezo wa wadau wa maendeleo wa sekta ya mchele umesamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba

Amri hii haujatolewa ikiwa magari tajwa yatatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafikia ukomo wa kutumika tarehe 16 ya mwezi Machi, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Chesesi | Namba ya injini |
|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J30-F024673 | 1HZ-1039749 |
| 2 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J90-F024760 | 1HZ-1040235 |
| 3 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J90-F024900 | 1HZ-1040878 |

Dodoma,
23 Januari, 2023.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*